268. E’YESU ingia rohoni kabisa

268

1. E’ Yesu, ingia rohoni kabisa, uniweke huru nakunitakasa, nipate kushirikiana na wewe katika mateso na raha daima!

Pambio:
:/: E’ Bwana, nijaze upendo wa mbingu nao uthabiti, niwe mshindaji! :/:

2. Siombi ufalme, siombi heshima, naomba kupewa neema daima, nijue ukweli wa neno la Mungu: Mtoe miili na iwe dhabihu!

3. Ingia rohoni, unichungulie, na katika yote unisaidie, nipate kabisa kusudi na nia kujitoa kwako, kukutumikia!

4. Hakuna la huku litanizuia nisifananishwe na Yesu Masiya. Nitumainije kufika mbinguni nisiposhiriki Mwokozi mpendwa!

Emil Gustavsson, 1892

O Jesus, min Jesus,